Soma mazungumzo kati ya Sungura na chui kisha ujibu maswali. **Sungura:** Habari za leo kaka chui?

Chui: Nzuri.

Sungura: Leo umekunywa maji?

Chui: Sijanywa maji.

Sungura: Ooh! Itabidi nimwagize pweza atuletee maji kutoka baharini. Leo bahari ni shwari."

Chui: Hapana. Kuna binadamu anayeitwa Ng'wale anauza maji.

Sungura: Inaonekana humpendi pweza.

Chui: Si kweli. Sina uadui na pweza.

Sungura: Nafikiri tuwaache wote. Tuagize maji kutoka kwa Kyando.

Chui: Nakubaliana na wewe. Maji anayouza Kyando ni safi sana.

Sungura: Kweli. Itabidi tununue hapo.

Chui: Sawa mdogo wangu.

Maswali

1. Sungura alimuuliza chui kama amekunywa nini?
   (Mwanafunzi ajibu)
2. Pweza alikuwa atoe wapi maji?
   (Mwanafunzi ajibu)
3. Binadamu yupi alikuwa anauza maji?
   (Mwanafunzi ajibu)
4. Waliyanunua maji ya nani?
   (Mwanafunzi ajibu)
5. Maji ya Kyando yalikuwaje?
   (Mwanafunzi ajibu)

SEHEMU YA 2: KUSOMA KWA SAUTI (ALAMA 10)

Soma hadithi hii kwa sauti.

Jamii ni watu wanaoishi pamoja na kushirikiana katika shughuli mbalimbali. Wema hutengeneza jamii bora. Ni vizuri kufahamu jinsi ya kuishi vizuri na wanajamii wengine. Ili kuishi vizuri na wanajamii wengine unapaswa kujipenda, kujitambua na kuwapenda wengine. Kujipenda ni kujidhamini na kujikubali. Mtoto anayejipenda anatunza afya yake. Vilevile, anaepuka matendo mabaya na anakuwa na tabia njema wakati wote. Mtoto mwema huwa baraka kwa wazazi wake na jamii. Mara nyingi mtoto mwema huwatii wakubwa wake. Akitumwa huenda bila kukasirika. Wanafunzi wengi wamefunzwa wema na adabu shuleni. Inawapasa kutumia mafunzo hayo kila mahali. Walimu na wazazi pia wanapaswa kuwa vielelezo bora katika jamii. Jamii bora watu huwa wema.

SEHEMU YA 3: UFAHAMU (ALAMA 1)

Ufahamu 1

Soma ufahamu huu kisha ujibu maswali.

Mwalimu Nyongesa anatufundisha uraia na maadili katika shule yetu ya Msingi Bora. Siku moja aliwataka wanafunzi wa darasa la tatu kueleza vipaji walivyonavyo. Kila mwanafunzi alipewa nafasi ya kujieleza. Amina na Jalima walisema kuwa wangeweza kuchora vizuri sana. Mwalimu aligundua Amina na Jalima ni hodari wa kuchora. Sara na Musa walijitokeza na kusema wangeweza kuimba vizuri sana. Miami na Zubera walisema kwamba wao wangeweza kucheza mpira wa miguu kwa ustadi. Hii ilimfahamisha Mwalimu Nyongesa kuwa wanafunzi wake walikuwa na vipaji tofauti. Baada ya hapo, aliweka mipango ya kukuza vipaji vya wanafunzi wake. Aliwasihi kila mmoja atie bidii katika kukuza kipaji alichokuwa nacho.